

# Kwenda kwenye sinema

 Espen Stranger-Johannessen

 Aakanee

 Jacob Haule

 3

 Kiswahili 



Mai anatafuta filamu ya kutazama. Anataka kwenda kwenye sinema na rafiki yake kipenzi, Lisa.



Mai anapanda skuta yake kwenda kwenye sinema.  
Wamekubaliana kukutana huko.



Huko kwenye sinema wanasalimiana. Wana shauku ya kutazama filamu.



Mai ananunua tiketi za wote wawili katika kaunta ya tiketi.



Pia ananunua popkorni nyingi.



Lisa anabeba popkorni wakati Mai ananunua chupa  
mbili za soda.



Wanaonesha tiketi zao kabla ya kuingia ndani  
kutazama filamu.



Wanatafuta viti vyao. Kuna giza kwa sababu filamu tayari imeanza.



Wanakaa chini ili watazame filamu.



Ni filamu ya mapenzi, ambayo ndiyo wanayoipenda zaidi.



Baada ya filamu wanaagana na kwenda nyumbani.



# LIDA Stories

[lidastories.net](http://lidastories.net)

## Kwenda kwenye sinema

✎ Espen Stranger-Johannessen

☒ Aakanee

♫ Jacob Haule

